



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na. F.10/3/VOL.III/57

27/10/2023

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA. LGA/NDC/088/C/2023/2024/02

ZABUNI ZA WAKALA WA UKUSANYAJI MAPATO KATIKA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU

1. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu inakusudia kuweka Mawakala wa kukusanya Mapato kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato kwa kipindi cha Mwaka wa fedha unaoendelea 2023/2024.
2. Kupitia tangazo hili Halmashauri inapenda kuwaalika watu binafsi, Makampuni, Mashirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia na uwezo wa kuingia mikataba ya kukusanya mapato kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo: -

NA.	CHANZO CHA MAPATO	NAMBA YA ZABUNI
1.	Ukusanyaji wa taka katika Mji wa Mangaka	LGA/NDC/088/C/2023/2024/02/1
2.	Uendeshaji wa huduma ya choo cha kulipia kilichopo eneo la Stendi ya Mabasi Mangaka	LGA/NDC/088/C/2023/2024/02/2
3.	Utozaji ushuru wa Magulio/Minada katika Wilaya ya Nanyumbu	LGA/NDC/088/C/2023/2024/02/3

Masharti kwa waombaji

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Mwombaji awe na uwezo wa kuweka amana (*Security bond*) ya miezi mitatu ya kiwango ambacho amependekeza kulipa kila mwezi.
3. Mwombaji kama ni mtu binafsi anatakiwa kuambatisha nakala ya kivuli cha Kitambulisho cha Taifa (**NIDA**) au Namba ya Kitambulisho cha Taifa.
4. Mwombaji Kama ni Kampuni iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
5. Mwombaji atakayeshinda zabuni atakusanya mapato kwa kuzingatia viwango vilivyopitishwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

6. Ombi la uwakala liwe na jina na anuani sahihi ya Mwombaji. Aidha Mwombaji aonyeshe mahali anapokaa (*Postal and Physical address should legibly and clearly be indicated*).
7. Mwombaji aambatishe nakala ya taarifa zake za Kibenki (*Bank Statement*) ya kipindi cha miezi sita mfululizo.
8. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri kwa kazi yoyote ile, na awe na uzoefu wa kutosha juu ya kazi anayoomba.
9. Mwombaji asiwe Mtumishi au Kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.
10. Mwombaji atawajibika kufanya usafi katika eneo atakalopewa kwa gharama zake kwa kipindi chote atakachofanya kazi
11. Mwombaji atalipa ada ya **Tshs. 50,000/=** kama ada ya maombi ya kazi na haitarudishwa (*None Refundable*). Malipo hayo yalipwe kwa Mkurugenzi Mtendaji S. L. P. 246, **NANYUMBU**.
12. Mwombaji atakayeshindwa kutimiza au kukamilisha maekelezo na masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye ushindani.
13. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ioneshwe namba ya Zabuni. Zabuni ziwasilishwe kwa mkono au kwa njia ya Posta kupitia anuani ifuatayo: -
Mkurugenzi wa Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 246,
NANYUMBU-MTWARA
14. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa barua barua **Pepe (e-mail)** hazitapokelewa.
15. Wenye nia ya kuomba zabuni hii wanaweza kupata taarifa za ziada katika ofisi ya Katibu - Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu Mkao Makuu, chumba Namba 24, kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 mchana, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko ya ki-Taifa
16. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 04/11/2023 saa nne kamili (4:00) asubuhi, na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kupokea zabuni hizo mbele ya waombaji watakao amua kuhudhuria kwenye ukumbi wa mikutano jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

Imetolewa na:



Ibrahim J. Mwanauta
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
NANYUMBU

